

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**MKOA WA NJOMBE**

Septemba 23, 2022

**NJOMBE**



**TAARIFA KWA UMMA**

Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka anatarajia kumpokea Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Balozi Dkt. Pindi H. Chana (Mb) Septemba 26, 2022 ambapo siku hiyo atazindua mkakati wa utangazaji Utalii katika Mikoa ya Kusini mwa Tanzania.

Uzinduzi wa Mkakati huo utakuwa tarehe 26 Septemba 2022 katika Ukumbi wa Halmashauri ya Mji Njombe kuanzia saa tatu kamili asubuhi ukiambatana na Maonesho ya siku mbili kuanzia tarehe 25-26 Septemba, 2022.

Aidha uzinduzi huo utahudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kitaifa wakiwemo Waheshimiwa Mabalози wa Angola, Balozi wa Zimbabwe, Wakuu wa Mikoa ya kusini, Makatibu Tawala wa Mikoa ya Kusini, Spika Mstaafu wa Bunge Mhe. Anna Makinda, Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Njombe, Viongozi wote wa Mkoa wa Njombe, Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Makampuni na Mashirika mbalimbali.

Pamoja na hayo Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka anawaalika Wananchi wote wa Mkoa wa Njombe na Watanzania wote kwa ujumla wake kuja kushiriki uzinduzi huo.

A handwritten signature in blue ink.

**Chrispin B. Kalinga**  
**Kaimu Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini**  
**MKOA WA NJOMBE.**